# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# OFISI YA RAIS

# TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

# HALMASHAURI YA WILAYA YA URAMBO

## TAARIFA YA MAFANIKIO YA SERIKALI YA AWAMU YA SITA.

## 1.0 MAELEZO MAFUPI KUHUSU WILAYA

Halmashauri ya Wilaya ya Urambo ni moja kati ya Halmashauri8 zinazounda Mkoa wa Tabora na ilianzishwa tarehe 1 Januari mwaka 1984. Halmashauri inapakana na Wilaya ya Kaliua kwa upande wa Magharibi, Mashariki wilaya ya Uyui, Kusini Mkoa wa Katavi na Kusini Mshariki Wilaya ya Sikonge.

### 1.1 ENEO

Wilaya ya Urambo ina ukubwa Kilometa za mraba 6,110 ambazo kati ya hizo asilimia 52.3 ni Misitu ya hifadhi, asilimia 0.9 ni maji, asilimia 12.9 malisho ya wanyama, asilimia 8.4 eneo linalofaa kwa kilimo na asilimia 25.5 ni eneo la nchi kavu ambalo halifai kwa kilimo. Makao Makuu ya Wilaya yapo katika Mji Mdogo wa Urambo, Mji wa Urambo unafikika kwa barabara, reli na ndege ndogo.

## 1.2 UTAWALA

Wilaya ya Urambo ina Jimbo 1 la uchaguzi, tarafa 2 kata 18 vijiji 59 na vitongoji 256. Mchanganuo wake ni kama ifuatavyo: -

**Jedwali Na 1. Maeneo ya kiutawala**

| Tarafa | Eneo (km2) | Kata | Vijiji | Vitongoji | % ya Eneo |
|---|---|---|---|---|---|
| Urambo | 2,749.5 | 13 | 40 | 181 | 45 |
| Ussoke | 3,360.5 | 5 | 19 | 75 | 55 |
| **Jumla** | **6,110** | **18** | **59** | **256** | **100** |

## 1.3.IDADI YA WATU:

Wilaya ya Urambo kwa mujibu wa Sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022 ina jumla ya watu **260,322**. Kati ya hao, Wanawake ni **132,898**sawa na **51.05%**. na Wanaume ni **127,424**sawa na **48.95%**ya watu wote.

## 1.4 SHUGHULI MUHIMU ZA KIUCHUMI.

Shughuli kuu za kiuchumi katika Wilaya ya Urambo ni Kilimo, Ufugaji nyuki na Ufugaji mifugo. Mazao ya kibiashara yanayolimwa Urambo ni Tumbaku, Alizeti, Pamba, Korosho na Karanga. Mazao ya chakula yanayolimwa Urambo ni Mpunga, Mahindi, Viazi vitamu, Mihogo na mazao ya bustani kama vile nyanya, vitunguu, kabichi na mboga za majani.

## 1.5 HALI YA ULINZI NA USALAMA

Hali ya Ulinzi na Usalama katika Wilaya ni ya kuridhisha kiasi cha kuwaruhusu wananchi kufanya shughuli zao za kujipatia kipato na kushiriki katika kazi za ujenzi wa Taifa na kuinua maendeleo yao ya Kiuchumi. Aidha matukio madogomadogo yanayojitokeza yanashughulikiwa na vyombo vya usalama kiasi cha kuweka mazingira salama kwa wananchi na mali zao.

## 1.6 UWAKILISHI/HALI YA KISIASA

Wilaya ya Urambo ina jimbo 1 la uchaguzi ambalo ni Urambo likiongozwa na Mhe: Margaret S. Sitta – CCM. Aidha Wilaya pia ina Waheshimiwa Madiwani 17 wakuchaguliwa na 6 wa viti maalumu wote kutoka Chama cha Mapinduzi(CCM) na Diwani 1 kutoka chama cha Upinzani-CHADEMA. Kwa ujumla hali ya kisiasa Wilayani ni tulivu na Chama cha Mapinduzi(CCM) kinakubalika kwa asilimia 99 katika Nyanja zote.

## 2.0 UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO

Wilaya ya Urambo imekuwaikitekelezakikamilifu Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020-2025 ambapo utekelezaji huu umesaidia sana katika kuchochea Maendeleo ya wananchi wa Wilaya yetu na ukuaji wa uchumi kwa ujumla. Kwa kipindi cha Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Mh. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jumhuri ya Muungano wa Tanzania Wilaya imejipatia mafanikio mbalimbali kwa kutekeleza miradi ya maendeleo kupitia sekta zake kama ifuatavyo:

### *SEKTA YA ELIMU*

Katika kipindi cha Uongozi wa Awamu ya sita hadi sasa Wilaya imefanikiwa kuboresha miundombinu ya elimu ikiwa ni adhima ya Serikali ya kutoa elimu bora kwa wote kwa kuhakikisha mazingira ya kujifunzia na kufundishia yanakuwa rafiki na salama. Katika kutekeleza mkakati wa kuhakikisha elimu inakuwa haki ya kila mtanzania, Serikali kupitia Halmashauri imetekeleza miradi mbalimbali ya ujenzi ikiwemo vyumba vya madarasakatika elimu ya msingi113, madarasa 202 katika elimu ya sekondari, nyumba za walimu 08 katika shule za msingi 09 katika shule za sekondari, Aidha wilaya imejenga jumla ya matundu 442ya vyoo katika shule za msingi na 30 katika shule za sekondari na mabweni 7. Katika kipindi hiki cha miaka mitatu, kupitia sekta ya elimu miradi mikubwa ifuatayo imetekelezwa:

***Ujenzi wa shule mpya Samia***.

Halmashauri kupitia mradi wa wafadhili wa serikali BOOST imejenga shule mpya ya msingi yenye mikondo 2 na madarasa ya elimu awali ya mfano. Ujenzi huu umegharimu jumla ya **TZS 561,100,000.00**na shule tayari imefunguliwa na imepokea wanafunzi

***Ujenzi wa shule mpya ya sekondari Igunguli***

Halmashauri kupitia mradi wa wafadhili wa serikali SEQUIP imejenga shule mpya ya Sekondari yenye mikondo 2 na miundombinu yote muhimu ikiwemo jingo la utawa, maabara zote, maktaba na jengo la TEHAMA. Ujenzi huu umegharimu jumla ya **TZS603,890,562.00**na shule tayari imefunguliwa na imepokea wanafunzi.

***Ujenzi wa shule mpya na nyumba nne sekondari ya Kasisi***

Halmashauri kupitia mradi wa wafadhili wa serikali SEQUIP imejenga shule mpya ya Sekondari yenye mikondo 2 na miundombinu yote muhimu ikiwemo jingo la utawa, maabara zote, maktaba na jengo la TEHAMA. Ujenzi huu umegharimu jumla ya **TZS603,890,562.00**na shule tayari imefunguliwa na imepokea wanafunzi.

Vilevile uwezeshaji wa shughuli nyingine za elimu zisizokuwa miundombinu zimetekelezwa ambapo jumla ya **TZS. 12,001,436,353.29** zimetolewaa.Baadhi ya miundombinu iliyotekelezwa ni kama invyoonekana katika picha hapa chini



**Madarasa katika shule mpya ya msingi SAMIA**



**Nyumba ya mwalimu katika shule ya sekondari Kasisi**



**Vyoo vya kisasa katika shule ya msingi Mapambano**

Kuongezeka kwa miundombinu ya elimu iliyoboreshwa kumechochea kwa kiasi kikubwa ongezeko la idadi ya wanafunzi wanaoandikishwa katika shule za msingi na sekondari. Kwa mfano idadi ya wanafunzi waliondikishwa darasa la kwanza hadi Februari mwaka 2024 ni 9100 ikilinganishwa na wanafunzi…..mwaka 2021 sawa na ongezeko la asilimia…… aidha idadi ya wanafunzi wa sekondari waliochaguliwa kidato cha kwanza mwaka 2024 ni 5396 ikilinganishwa na wanafunzi 4076 mwaka 2021 sawa na ongezeko la asilimia 32%

***SEKTA YA AFYA***

Katika kipindi cha Uongozi wa Awamu ya sita hadi sasa Wilaya imeweza kutekeleza miradi mbalimbali ya ujenzi ikiwemo vituo vya afya vitatu, zahanatinane na nyumba za watumishi 6. Vilevile Halmashauri imefanikiwa kufanya ukarabati wa miundombinu mbalimbali katika Hospitali ya Wilaya, vituo vya afya na zahanati zake. Aidha serikaliimeiwezesha Wilaya kufanya manunuzi ya vifaa tiba na vitendanishi vya kutosha kwa ajili ya vituo vya kutolea huduma za afya. Katika utekelezaji wa shughuli hizi, jumla ya **Tsh 4,407,000,000.00**zimetolewa kwa ajili ya kutekelezamiradihiyo na ujenzi wa miradi mingi umekamilika wakati michache ipo katika hatua mbalimbali za ukamilishaji. Aidha Halmashauri imefanikiwa kupunguza vifo vya mama na mtoto kutoka asilimia…….hadi asilimia….. hii imetokana na uboreshaji wa huduma za afya uliopatikana kutokana na ujenzi na ununuzi wa vifaatiba katika vituo vyetu vya kutolea

huduma za afya. Baadhi ya miundombinu iliyotekelezwa katika sekta ya afya ni kama invyoonekana katika picha hapa chini



**Jengo jipya la maabara katika Hospitali ya Wilaya**



***Kichomea taka katika kituo cha afya Vumilia***



***Jengola huduma za wagonjwa wa nje(OPD) katika kituo cha afya Vumilia***



***Vifaa tiba(Vitanda) katika kituo cha afya Usoke mlimani***

***SEKTA YA MAENDELEO YA JAMII***

Wilaya imeendela kuweka mazingira rafiki kwa makundi mbalimbali kuweza kujiinua kiuchumi, Kipaumbele kimeelekezwa kwa makundi ya Wanawake, Vijana na watu wenye ulemavu kwa kuwapatia mikopo isiyo na riba. Katika kipindi cha uongozi wa awamu ya sita Wilaya kupitia makusanyo ya mapato ya ndani ya Halmashauri imeendelea kutenga asimilia 10 ya makusanyo yake kwa ajili ya kuwezesha mikopo

kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu , ambapo jumla ya **TZS.437,684,260.00** zimekwishatolewa kwa ajili ya vikundi vilivyokidhi vigezo na kustahili kupewa mkopo.

Aidha kupitia Mpango wa kunusuru kaya maskini -TASAF katika kipindi cha mitatuserikali imewezesha malipo kwa kaya masikini ambapo jumla ya **TZS.2,403,220,954.00** zimetumika katika kuhakikisha kaya hizo zinajikwamua kutoka katika hali ya umaskini uliokithiri.

***SEKTA YA KILIMO***

Katika kipindi cha uongozi wa Mh. Samia Suluhu Hassan, Serikali imefanya mabadiliko makubwa sana katika sekta ya kilimo ambapo imeboresha mazingira ya uzalishaji wa mazao ya kilimo na upatikanji wa chakula kwa kufanya mambo kadhaa kama ifuatavyo;

***Kuweka Ruzuku Kwenye Pembejeo Za Kilimo***

Serikali imefanikiwa kushusha bei ya mbolea kutoka TZS. 165,000.00 kwa mfuko wa Kg 50 msimu wa 2020/2021 hadi TZS. 70,000.00 kwa Msimu 2023/2024.

Aidha bei ya Mahindi ambayo ndiyo chakula kikuu katika Wilaya yetu imeshushwa kutoka TZS 1,250 kwa kilo hadi TZS 845 kutokana na Serikali kuleta mahindi ya Bei nafuu kutoka NFRA ambapo jumla ya tani 953.6 zililetwa mwaka 2022. Maamuzi haya ya kushusha bei ya mahindi mwaka 2022 yaliwezesha wakulima kupata chakula na hivyo kuweza kuzalisha ambapo katika msimu 2023/2024 hakuna uhaba kabisa wa chakula.

***Kuongeza uzalishaji na bei ya zao la tumbaku***

Makampuni ya kununua tumbaku yameongeza kiasi cha tumbaku kinachotakiwa kuzalishwa na wakulima wake kutoka kilo 6,033,000 msimu 2020/2021 hadi kilo 20,500,000msimu 2023/2024 hivyo kuongeza fursa ya wakulima kuongeza kipato.

Aidha Bei ya wastani ya serikali kwa makampuni kununua tumbaku iliongezeka kutoka USD 1.75 ya msimu 2021/2022 hadi USD 2.00 msimu 2022/2023 ambapo kutokana na ushindani, makampuni yameweza kununua tumbaku kwa bei ya wastani wa USD 2.21 kwa kilo kwa tumbaku iliyozalishwa msimu 2022/2023.

***SEKTA YA MIFUGO***

Katika kipindi cha uongozi wa awamu ya sita,Wilaya imefanikiwa kujenga na kuimarisha miundombinu katika sekta ya mifugo ikiwemo ujenzi wa uzio wa mnada wa mifugo wa Urambo mjini wenye urefu wa mita 1,183na ujenzi wa josho pamoja na kipandishio cha wanyama kwa thamani ya **Tsh 168,973,507.00**ikiwa ni fedha kutoka mapato ya ndani ya Halmashauri. Aidha Wilaya imefanikiwa kujenga uzio wa mnada mwingine wa mifugo katika kijiji cha Ukwanga kwa usimamizi wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi ambapo jumla ya **TZS. 252,000,000.00** zimetumika.



**Uzio wa mnada wa mifugo katika kijiji cha Ukwanga**

**HALI YA UKUSANYAJI WA MAPATO**

Hali ya ukusanyaji wa mapato ya Halmashauri ya Wilayaimekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka kutoka kiasi cha2,417,780,346.18mwaka 2021/22 sawa na asilimia 88.32, kiasi cha 2,669,159,104 mwaka 2022/2 Sawa na 86.3% na kiasi cha 3,011,787,773.82 mwaka 2023/2024 hadi Februali sawa na 86.3% kati 3,491,270,000.00 ya makisio . Ongezeko hili la mapato limeiwezesha Halmashauri kuanzisha kiwanda cha ufyatuaji wa matofali kwa lengo la kuboresha na kuongeza ubora wa majengo yanyojengwa na miradi ya Serikali



**Kiwanda cha uzalishaji wa matofari ya Halmashauri-Urambo**

**CHANGAMOTO**

Katika utekelezaji wa shughuli mbalimbali, Wilaya ya Urambo inakabiriana na changamoto mbalimbali ikiwemo;

- Ukosefu wa maji safi na salama ya uhakika. Wilaya kwa sehemu kubwa imethibitika kuwa na miamba isiyotoa maji ya kutosha na hivyo kukwamisha jitahada za serikali katika kuondoa kero ya maji kwa wananchi
- Ukosefu wa umeme wa uhakika unaosababishwa na kukatika kwa mara kwa mara
- Uhaba mkubwa wa watumishi hususani katika sekta ya afya na elimu

**UTATUZI WA CHANGAMOTO**

Katika kukabiliana na changamoto kubwa zilizopo, Wilaya kupitia sekta zake inaendelea kuchukua hatua kadhaa kama vile;

- Ujenzi wa mradi mkubwa wa maji kutoka ziwa Viktoria. Mradi huu ambao tayari mkandarasi yuko saiti kukamilika kwake kutakuwa suluhisho la kudumu la uhaba wa maji safi na salama katika Wilaya yetu.
- Mradi wa ujenzi wa kituo kikubwa cha kupozea umeme unaojengwa katika kijiji cha Uhuru Kata ya vumilia. Kukamilika kwa mradi huu ikiwa ni pamoja na

ubadilishaji wa miundombinu ya usafirishaji wa umeme itakuwa suluhisho la kudumu la kiasi cha umeme na utulivu wake.

- Kuomba mamlaka za ajira kutoa vibali vya ajira kulingana na takwimu zinazowasilishwa kuhusu hali ya watumishi ndani ya Wilaya.

**HITIMISHO**

Napenda kuchukua nafasi hii kwa heshima na taadhima, kumshukuru na kumpongeza Mh. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa juhudi zake za kuleta maendeleo kwa nchi na jamii kwa ujumlakupitia sekta za Elimu, Afya, Maji na sekta zote za kiuchumi zinazogusa maisha ya wananchi moja kwa moja.

Nawasilisha

Grace S. Quintine

**MKURUGENZI MTENDAJI(W)**

**URAMBO**